**HALMASHAURI YA WILAYA LONGIDO.**

S.L.P 84
LONGIDO,
MKOA WA ARUSHA.

Barua zote ziandikwe kwa
Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya wilaya Longido
Simu No. 027 – 2539603/2

Unapojibu tafadhali taja:
**KUMB. NA HW/LONG/B/02/91**

**13/07/2023**

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido anawatangazia Nafasi za Kazi (Mkataba wa muda mfupi) na anakaribisha maombi ya Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi hizo kama ifuatavyo:-

## 1.0 WAKUSANYA USHURU WA MINADA (NAFASI 10).

Nafasi hii ni kwa ajili ya Minada ya Irkaswa, Olmolog, Sinya, Ngereyani, Tingatinga, Orbomba, Kiserian, Engikareth, Mivaf, Ketumbeine, Noondoto, Gilai Lumbwa, Gilai Mergoi, Engaranaibor, Mundarara, Wosiwosi, Olturooibor(Matale B) na Alakirikir (Matale A).

### 1.1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa mwenye Elimu kuanzia kidato cha nne (IV) au kidato cha sita (VI) au cheti cha taaluma kuanzia ngazi ya Astashahada hadi shahada kutoka katika vyuo vinavyotambulika na serikali.

### 1.1.2 MAJUKUMU YA KAZI

- Kukusanya ushuru wa Ng'ombe wa Tshs 7,500 kwa kila ng'ombe anayeuzwa mnadani,
- Kukusanya ushuru wa mbuzi/kondoo wa Tshs 3,000 kwa kila mbuzi/kondoo anayeuzwa mnadani.
- Kuweka fedha benki kila siku baada ya makusanyo,

CamScanner

- Kuwasilisha ripoti za makusanyo na uwekaji wa fedha benki Ofisi ya Mkurugenzi kila mwisho wa juma,
- Kutoza faini kwa wachuuzi wanaokiuka taratibu za minada kwenye masoko.

### 1.1.3 MSHAHARA

Kwa wanaokusanya zaidi ya Milioni mbili kwa mwezi watalipwa mshahara wa Tshs 300,000 na minada inayokusanya chini ya Milioni mbili kwa mwezi watalipwa asilimia 15 ya walichokusanya kwa mwezi.

## 2.0 WAKUSANYA USHURU WA MAZAO NA USAFI WA MAZINGIRA (NAFASI 5).

Nafasi hii ni kwa maeneo ya Longido, Kamwanga na Olmolog

### 2.1 SIFA ZA MWOMBAJI.

Kuajiriwa mwenye Elimu kuanzia kidato cha nne (IV) au kidato cha sita (VI) au cheti cha taaluma kuanzia ngazi ya Astashahada hadi shahada kutoka katika vyuo vinavyotambulika na serikali.

### 2.1.1 MAJUKUMU YA KAZI.

- Kukusanya ushuru wa mazao ya kilimo (Produce cees),
- Kukusanya ushuru wa Magari makubwa kwa ajili ya usafi wa mazingira
- Kuweka kumbukumbu ya Idadi ya Malori yanayopita kwa siku,
- Kutoa taarifa ya Makusanyo ya Fedha za mazao kwa siku na mwezi,
- Kuweka fedha benki kila siku baada ya makusanyo,
- Kuwasilisha ripoti za makusanyo na uwekaji wa fedha benki Ofisi ya Mkurugenzi kila mwisho wa juma,
- Kutoza faini kwa wafanyabiashara wanaokiuka taratibu.

CamScanner

### 2.1.3 MSHAHARA.

Mshahara utakuwa ni Tshs 300,000 kwa mwezi.

## 3.0 WAKUSANYA USHURU WA MADINI YA UJENZI – MORAMU, MAWE NA MCHANGA (NAFASI 5)

Nafasi hii ni kwa maeneo ya Longido, Engasurai, Oltepes, Engaranaibor, Ketumbeine na Namanga.

### 3.1 SIFA ZA MWOMBAJI.

Kuajiriwa mwenye Elimu kuanzia kidato cha nne (IV) au kidato cha sita (VI) au cheti cha taaluma kuanzia ngazi ya Astashahada hadi shahada kutoka katika vyuo vinavyotambulika na serikali.

### 3.1.1 MAJUKUMU YA KAZI.

- Kukata ushuru wa kokoto na mchanga kwa viwango vya Tshs 15,000 kwa gari la tani 7 na 30,000 kwa gari la zaidi ya tani 7.
- Kutoa taarifa ya Makusanyo ya Fedha za mazao ya maliasili kwa siku na mwezi,
- Kuweka fedha benki kila siku baada ya makusanyo,
- Kuwasilisha ripoti za makusanyo na uwekaji wa fedha benki Ofisi ya Mkurugenzi kila mwisho wa juma,
- Kutoza faini kwa wafanyabiashara wanaokiuka taratibu.

### 3.1.2 MSHAHARA.

Kwa wanaokusanya zaidi ya Milioni mbili kwa mwezi watalipwa mshahara wa Tshs 300,000 na Makusanyo chini ya Milioni mbili kwa mwezi watalipwa asilimia 15 ya walichokusanya kwa mwezi.

CamScanner

## 4.0 WANAOKUSANYA USHURU WA GETI LA UTALII (NAFASI 2)

Nafasi hii ni kwa eneo la Oldonyolengai.

### 4.1 SIFA ZA MWOMBAJI.

Kuajiriwa mwenye Elimu kuanzia kidato cha nne (IV) au kidato cha sita (VI) au cheti cha taaluma kuanzia ngazi ya Astashahada hadi shahada kutoka katika vyuo vinavyotambulika na serikali.

### 4.1.2 MAJUKUMU YA KAZI.

- Kutoza kila Mtalii kwa kiwango cha Tshs 11,000 kwa mtu mwenye umri wa chini ya miaka 18 na Tshs 22,000 kwa mtalii mwenye umri zaidi ya miaka 18
- Kuhakikisha kwamba anapeleka fedha benki.
- Kuwasilisha ripoti za wageni walioingia na kiasi cha makusanyo Ofisi ya Mkurugenzi kila mwisho wa juma,
- Kutoza faini kwa madereva wanaokiuka taratibu.

### 4.1.3 MSHAHARA.

Mshahara utakuwa ni Tshs 300,000 kwa mwezi.

## 5.0 WAKUSANYA USHURU WA MAGULIO. (NAFASI 4)

Nafasi hii ni kwa Tarafa za Ketumbeine, Engarenaibor, Longido na Enduimet

### 5.1 SIFA ZA MWOMBAJI.

Kuajiriwa mwenye Elimu kuanzia kidato cha nne (IV) au kidato cha sita (VI) au cheti cha taaluma kuanzia ngazi ya Astashahada hadi shahada kutoka katika vyuo vinavyotambulika na serikali.

### 5.1.2 MAJUKUMU YA KAZI.

- Kukata ushuru wa bidhaa kwa wafanyabiashara wote wasio na vitambulisho vya ujasiriamali,
- Kuweka fedha benki kila siku baada ya makusanyo,

CS CamScanner

CS CamScanner

- Kuwasilisha ripoti za makusanyo na uwekaji wa fedha benki Ofisi ya Mkurugenzi kila mwisho wa juma,
- Kutoza faini kwa wafanyabiashara wanaokiuka taratibu.

### 5.1.3 MSHAHARA.

Kwa wanaokusanya zaidi ya Milioni mbili kwa mwezi watalipwa mshahara wa Tshs 300,000 na Makusanyo chini ya Milioni mbili kwa mwezi watalipwa asilimia 15 ya walichokusanya kwa mwezi.

## 6.0 USHURU WA STENDI YA ABIRIA. (NAFASI 1)

Nafasi hii ni kwa stendi ya Longido.

### 6.1 SIFA ZA MWOMBAJI.

Kuajiriwa mwenye Elimu kuanzia kidato cha nne (IV) au kidato cha sita (VI) au cheti cha taaluma kuanzia ngazi ya Astashahada hadi shahada kutoka katika vyuo vinavyotambulika na serikali.

### 6.1.1 MAJUKUMU YA KAZI.

- Kuwepo eneo lako la kazi (Stendi) kila siku kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni.
- Kuhakikisha kila gari linalipo tozo ya stendi kwa viwango vilivyoelekezwa.
- Kutoa risiti halali kwa magari yanapotoka yote
- Kuhakikisha unapokea fedha kabla ya kutoa risiti.
- Kuhakikisha hakuna gari linalotoka stendi bila ya kulipa ushuru.
- Kuandaa taarifa ya makusanyo na uwekeji fedha ya wiki na kuiwasilisha Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya.

CamScanner

## 7.0 MAEGESHO YA MALORI (LORY PARKING) (NAFASI 5)

Nafasi hii ni kwa eneo la Longido, Eworendeke Namanga

### 7.1 SIFA ZA MWOMBAJI.

Kuajiriwa mwenye Elimu kuanzia kidato cha nne (IV) au kidato cha sita (VI) au cheti cha taaluma kuanzia ngazi ya Astashahada hadi shahada kutoka katika vyuo vinavyotambulika na serikali.

### 7.2 MAJUKUMU YA KAZI.

- Kuwepo kwenye stendi ya maegesho muda wote wa masaa yako ya kazi uliyopangiwa.
- Kutoza tozo ya Tshs 5,000 kwa siku kwa kila gari kubwa lililopo ndani ya maegesho,
- Kutoza magari madogo na makubwa yanayopaki kwenye maeneo rasmi ya maegesho
- Kutoa risiti halali kwa magari yote yatakayotozwa,
- Kuandaa taarifa za makusanyo na za uwekaji wa fedha benki na kuiwasilisha benki kila mwisho wa juma.

### 7.3 MSHAHARA.

Kwa wanaokusanya zaidi ya Milioni mbili kwa mwezi watalipwa mshahara wa Tshs 300,000 na Makusanyo chini ya Milioni mbili kwa mwezi watalipwa asilimia 15 ya walichokusanya kwa mwezi.

## MASHARTI YA JUMLA.

i. Mwombaji awe na umri usiozidi miaka 45

ii. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayo jitosheleza (Detailed C.V)

iii. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, vyeti vya elimu, cheti cha kuzaliwa na picha mbili za rangi za hivi karibuni (Passport Size) na kila picha iandikwe jina nyuma.

CamScanner
CamScanner

iv. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU na NECTA).

V. Uwasilishaji wa taarifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za kesheria.

vi. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **26 Julai, 2023 saa 9:30** Masjala Bayana ya Halmashauri ya Wilaya ya Longido.

viii. **Maombi yanaweza kuandikwa kwa Lugha ya Kiswahili au Kiingereza na kuwasilishwa Masjala bayana ya Halmashauri ya Wilaya ya Longido au kwa njia ya posta kwa kutumia anwani ifuatayo.**

**MKURUGENZI MTENDAJI,**
**HALMASHAURI YA WILAYA,**
**S. L. P. 84,**
**LONGIDO.**

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
P.O.BOX 84 LONGIDO
LONGIDO DISTRICT COUNCIL

**Stephen A. ULAYA,**
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAUI YA WILAYA YA LONGIDO.**

CamScanner